



# **UTAFITI WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAYA BINAFSI 2017 - 18**

## **MATOKEO YA VIASHIRIA MUHIMU**

Dodoma, Juni 2019





Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# Matokeo ya Viashiria Muhimu

**Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya  
Binafsi kwa Tanzania Bara, 2017-18**

Ofisi ya Taifa ya Takwimu  
Wizara ya Fedha na Mipango

Juni, 2019



Global Affairs  
Canada



Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Kwa Tanzania Bara wa Mwaka 2017-18 ulifanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ikishirikiana na Idara ya Kuondoa Umaskini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Utafiti huu ulipata fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Wadau wa Maendeleo ambao ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UN Women), Ubalizi wa Ireland, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF) na Shirika la Msaada la Canada (GAC). Msaada wa kitaalam ulitolewa na WB, UN Women na UNICEF.

Taarifa zaidi kuhusu Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017-18 zinapatikana katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Makao Makuu, Barabara ya Jakaya Kikwete; S. L. P. 2683, Dodoma, Tanzania. Simu: +255 26 - 2963822; Nukushi: +255 26 - 2963828; Barua Pepe: [sg@nbs.go.tz](mailto:sg@nbs.go.tz) na Tovuti: <http://www.nbs.go.tz>.

**Namna ya Kunukuu Ripoti Hii:**

Wizara ya Fedha na Mipango - Idara ya Kuondoa Umaskini [Tanzania Bara] na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), 2019. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017-18. Viashiria Muhimu. Dodoma, Tanzania.

## Yaliyomo

Orodha ya Majedwali .....	ii
Orodha ya Michoro .....	iii
Dibaji .....	iv
Shukrani .....	v
1 UTANGULIZI .....	1
1.1 Malengo ya Utafiti .....	1
2 UTEKELEZAJI WA UTAFITI .....	3
2.1 Muundo wa Sampuli .....	3
2.2 Maboresho .....	3
2.3 Madodoso .....	4
2.4 Utafiti wa Majaribio .....	5
2.5 Uorodheshaji wa Kaya, Ajira ya Wadadisi na Mafunzo .....	5
2.6 Ukusanyaji wa Taarifa .....	5
2.7 Uchakataji wa Taarifa .....	5
2.8 Mwitikio wa Utafiti .....	5
3 UPIMAJI WA KIWANGO CHA UMASKINI .....	6
3.1 Fahirisi za Umaskini .....	6
4 VIASHIRIA MUHIMU .....	8
4.1 Muundo wa Matumizi .....	8
4.2 Mstari wa Umaskini .....	9
4.3 Kiwango na Kina cha Umaskini .....	9
4.4 Mwenendo wa Umaskini; .....	11
4.5 Mgawanyo wa Watu Maskini .....	11
4.6 Umaskini na Muundo wa Kaya .....	13
4.6.1 Umaskini kwa Idadi ya Wanakaya .....	13
4.6.2 Umaskini kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya .....	14
4.7 Tofauti ya Kipato .....	14
5 VIASHIRIA VYA UMASKINI VISIVYO VYA KIPATO .....	15
5.1 Muundo wa Kaya .....	15
5.1.1 Wastani wa Ukubwa wa Kaya .....	15
5.1.2 Uwiano wa Wanakaya Tegemezi .....	16
5.2 Hali ya Makazi .....	17
5.3 Matumizi ya Umeme .....	18
5.4 Matumizi ya Nishati .....	20
5.4.1 Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kuangazia .....	20
5.4.2 Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kupikia .....	21
5.5 Huduma ya Maji .....	22
5.6 Huduma za Vyoo .....	23
5.7 Umiliki wa Akaunti za Benki .....	24

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 4.1:	Wastani wa Matumizi ya Kaya na Wastani wa Matumizi ya Mtu Mzima kwa Mwezi kwa Eneo, Mkoa na Aina ya Wastani ya Matumizi, Tanzania Bara, HBS 2017-18 .....	8
Jedwali Na. 4.2:	Mstari wa Umaskini wa Chakula na Mahitaji ya Msingi (shilingi) kwa Mtu Mzima kwa mwezi, Tanzania Bara, HBS 1991-92 hadi 2017-18.....	9
Jedwali Na. 4.3:	Viwango vya Umaskini kwa Eneo na Mkoa, Tanzania Bara, HBS 2017-18.....	10
Jedwali Na. 4.4:	Kiwango cha Umaskini kwa Idadi ya Wanakaya na Aina ya Umaskini, Tanzania Bara, HBS 2017-18 .....	13
Jedwali Na. 4.5:	Kiwango cha Umaskini kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya na Aina ya Umaskini, Tanzania Bara, HBS 2017-18 .....	14
Jedwali Na. 4.6:	Mwelekeo wa Kipimo cha GINI kwa Eneo, Tanzania Bara, HBS 2017-18.....	14
Jedwali Na. 5.1:	Wastani wa Ukubwa wa Kaya kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo na Mkoa, Tanzania Bara, HBS 2017-18.....	15
Jedwali Na. 5.2:	Asilimia ya Tegemezi na Wasiyo Tegemezi kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo na Mkoa, Tanzania Bara, HBS 2017-18.....	16
Jedwali Na. 5.3:	Asilimia ya Kaya Zenye Nyumba Zilizojengwa kwa Kutumia Vifaa vya Ujenzi vya Kisasa kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo, Mkoa na Aina ya vifaa vya Ujenzi, Tanzania Bara, HBS 2017-18 .....	18
Jedwali Na. 5.4:	Asilimia ya Kaya ambazo Jengo Kuu Limeunganishwa kwenye Umeme kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo na Mkoa, Tanzania Bara, HBS 2017-18.....	19
Jedwali Na. 5.5:	Mgawanyo (asilimia) wa Kaya kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo, Mikoa na Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kuangazia, Tanzania Bara, HBS 2017-18.....	20
Jedwali Na. 5.6:	Mgawanyo (asilimia) wa Kaya kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo, Mkoa na Chanzo Kikuu cha Nishati ya Kupikia, Tanzania Bara, HBS 2017-18.....	21
Jedwali Na. 5.7:	Asilimia ya Kaya Zenye Chanzo Kikuu cha Maji Kilichoboreshwa Wakati wa Msimu wa Mvua na Kiangazi kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo na Mkoa, Tanzania Bara, HBS 2017-18.....	22
Jedwali Na. 5.8:	Asilimia ya Kaya Zinazotumia Vyoo Visivyoboreshwa na Vilivyoboreshwa kwa Jinsi ya Mkuu wa Kaya, Eneo na Mikoa, Tanzania Bara, HBS 2017-18 .....	23
Jedwali Na. 5.9:	Asilimia ya Kaya Zilizo na Mwanakaya Mwenye Akaunti Benki kwa Mkoa, Tanzania Bara, HBS 2017-18.....	25

## Orodha ya Michoro

Mchoro Na. 4.1:	Mwelekeo wa Umaskini, Tanzania Bara, HBS 2011-12 na 2017-18...	11
Mchoro Na. 4.2:	Mgawanyo (asilimia) wa maskini wa mahitaji ya msingi kwa Eneo, Tanzania Bara, HBSs 2011-12 na 2017-18 .....	12
Mchoro Na. 5.1:	Asilimia ya Kaya Zenye Nyumba Zilizojengwa kwa Kutumia Vifaa vya Ujenzi vya Kisasa kwa Aina ya Vifaa, Tanzania Bara, HBS 1991-92 hadi 2017-18 .....	17
Mchoro Na. 5.2:	Asilimia ya Kaya ambazo Jengo Kuu Limeunganishwa kwenye Umeme, Tanzania Bara, HBS 2017-18 .....	19
Mchoro Na. 5.3:	Asilimia ya Kaya Zinazotumia vyoo vilivyoboreshwa kwa Mkoa, Tanzania Bara, HBS 2018-17 .....	24
Mchoro Na. 5.4:	Asilimia ya Kaya Zilizo na Mwanakaya Mwenye Akaunti Benki kwa Mkoa, Tanzania Bara, HBS 2017-18.....	26





## *Dibaji*

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2017-18 ni utafiti wa tano kufanyika kisayansi katika mfululizo wa tafiti zilizofanyika Tanzania Bara tangu mwaka 1991-92. Utafiti wa HBS 2017-18 ulifanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango.



Mhe. Dkt. Philip I. Mpango (Mb.)  
**Waziri wa Fedha na Mipango**

Lengo kuu la HBS 2017-18 ni kupata taarifa za sasa za hali ya umaskini na viashiria vinavyohusiana na umaskini na kupima maendeleo yaliyofikiwa katika kuimarisha hali ya maisha ya watu. Matokeo ya utafiti yatatumika katika kufuatilia, kupima na kutathmini utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo kitaifa, kikanda na kimataifa hususan Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo (2016/17 - 2020/21), Dira ya Africa Mashariki ya 2050, Agenda ya Afrika ya mwaka 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030 (SDGs). Taarifa hii inatoa Viashiria Muhimu vya Utafiti. Taarifa ya kina ya utafiti huu itatolewa rasmi mwezi Desemba 2019.

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2017-18 ulishirikisha wadau kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali pamoja na Washirika wa Maendeleo wakiongozwa na Benki ya Dunia.

Ni matumaini yangu kwamba, taarifa hii ya viashiria muhimu itawawezesha watunga sera, mameneja wa programu mbalimbali na wadau wengine kupata taarifa muhimu wanazohitaji katika utekelezaji wa majukumu yao wakati wakisubiri maelezo zaidi kuhusu utafiti wa HBS 2017-18.

Mhe. Dkt. Philip I. Mpango (Mb.)  
**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO**



## Shukrani

Ripoti ya Viashiria Muhimu inaonesha viashiria vya umasikini kwa mwaka 2017-18. Mafanikio ya Utafiti huu ni matokeo ya ushirikiano na mchango wa watu binafsi na taasisi mbalimbali. Nitumie fursa hii kutoa shukrani za dhiti kwa watu wote na taasisi zilizoshiriki katika kuhakikisha kwamba Utafiti huu umefanikiwa hadi kutoa Muhtsari wa Matokeo Muhimu kwa wadau wote wakati tukiendelea na uchambuzi wa kina.



Dkt. Albina Chuwa  
Mtakwimu Mkuu wa Serikali  
Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Shukrani zangu ziende kwanza kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Benki ya Dunia, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UN Women), Ubalizi wa Ireland, Ubalizi wa Sweden, UNICEF na Shirika la Misaada la Canada kwa msaada wao wa kifedha na utaalamu katika kutekeleza Utafiti huu. Serikali inathamini michango iliyotolewa na Wadau wa Maendeleo katika kufanikisha Utafiti wa HBS 2017-18.

Pia napenda kuwashukuru wataalam wote kutoka ndani na nje ya Nchi hususan Dkt. Richard Valliant, mshauri wa kimataifa katika uandaaji wa sampuli ya utafiti, Dkt. Sasun Tsirunyan mshauri wa kimataifa katika uchambuzi wa viashiria vya umaskini na Bw. Sango Simba mshauri wa ndani wa ukaguzi wa ubora wa takwimu kwa mchango wao katika kuhakikisha utafiti unafanyika katika ubora unaokubalika. Vile vile, ningependa kutambua mchango wa wajumbe mbalimbali wa kamati ya kitaalamu ya HBS 2017-18 ambao walihakikisha kuwa utafiti unafanikiwa. Napenda kushukuru utaalam uliotolewa na Benki ya Dunia katika hatua zote za maandalizi na utekelezaji wa utafiti hususan Idara inayoshughulika na uchambuzi wa masuala ya umaskini ukiongozwa na Nadia Belhaj Hassine. Mwisho, napenda kuwashukuru wanakaya wote katika kaya zilizochaguliwa kwa kutoa ushirikiano wakati wa utafiti.

Dkt. Albina Chuwa  
**MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**



# 1 UTANGULIZI

Tanzania Bara, kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu imekuwa ikifanya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi kama chanzo kikuu cha taarifa za mapato, matumizi na hali ya umaskini nchini tangu mwaka 1969. Utafiti wa kwanza wa kisayansi, uliohusisha maeneo ya mijini na vijijini, ulifanyika mwaka 1991-92. Hadi mwaka 2018, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanya tafiti tano za kisayansi za mapato na matumizi ya kaya binafsi. Taarifa za tafiti hizi ni chanzo kikuu cha makadirio ya viashiria vya umaskini na mienendo yake. Pia tafiti za HBS zinatoa takwimu zinazoweza kusaidia wadau kuelewa suala zima la umaskini wa kipato (kwa kutumia matumizi kama mbadala wa kipato).

Katika kutekeleza Utafiti huu, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (**NBS**), ilishirikiana na Idara ya Kuondoa Umaskini ya Wizara ya Fedha na Mipango -.Taasisi nyingine zilizoshiriki ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (**TAMISEMI**); Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Benki Kuu ya Tanzania (**BOT**); Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi; Taasisi ya Chakula na Lishe (**TFNC**); ESRF; REPOA; Idara ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika; Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (**NHIF**); Benki ya Dunia (**WB**); UN Women; Shirika la Maendelo la Umoja wa Mataifa (**UNDP**); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Idadi ya Watu (**UNFPA**); Ubalozi wa Ireland; Ubalozi wa Sweden; Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Watoto (**UNICEF**); na Shirika la Misaada la Canada (**GAC**).

Msaada wa kitaalam katika Utafiti huu ulitolewa na Benki ya Dunia, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF) na UN-Women.

Fedha za utekelezaji wa Utafiti huu zilitolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wadau wa Maendeleo; (Benki ya Dunia, UN Women, Ubalozi wa Ireland, Ubalozi wa Sweden, Shirika la Misaada la Canada na UNICEF).

## 1.1 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la HBS 2017-18 ni kupata taarifa za sasa za makadirio ya viwango vya umaskini na masuala yanayohusiana na umaskini kwa ajili ya kufuatilia, kupima na kutathmini mipango mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21), Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030 (SDGs 2030).

Malengo mengine ya utafiti wa HBS ni pamoja na;

- a) Kutoa mfululizo wa takwimu kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini hali na mwenendo wa umaskini ili kujua mabadiliko ya hali za maisha katika kaya, matokeo ya sera za kiuchumi, kijamii na ustawi wa watu;
- b) Kutoa taarifa za msingi za mapato na matumizi ya kaya kama ilivyoainishwa katika mfumo wa Pato la Taifa (GDP) na mfumo ya Pato la Taifa; na
- c) Kuhuisha kizio cha takwimu za Pato la Taifa (GDP) na Fahirisi za Bei (CPI).

## 2 UTEKELEZAJI WA UTAFITI

Maandalizi ya HBS 2017-18 yalianza Julai mwaka 2016 kwa kuanzisha Kamati ya Wataalam yenye wajumbe kutoka Wizara, Idara na Wakala wa Serikali pamoja na Wadau wa Maendeleo. Kamati ya wataalam ilikuwa na jukumu la kutoa utaalum na msaada wa kifedha kwa ajili ya kutekeleza Utafiti huu.

### 2.1 Muundo wa Sampuli

Sampuli ya HBS 2017-18 ilihusisha watu kutoka katika kaya binafsi 9,552. Sampuli hii iliruhusu makadirio ya viashiria katika ngazi ya Mkoa na kwa maeneo ya Mijini na Vijijini katika ngazi ya Kitaifa.

Sampuli ya HBS 2017-18 ilichaguliwa katika hatua mbili. Hatua ya kwanza ilihusika na uchaguzi wa maeneo ya kuhesabia watu kutokana na orodha ya maeneo ya kuhesabia watu iliyoandaliwa wakati wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012. Jumla ya Maeneo 796 yalichaguliwa kitaalam (maeneo 69 kutoka Dar es Salaam, 167 kutoka Miji mingine na maeneo 560 kutoka Vijijini). Kabla ya kuchagua kaya kwa ajili ya Utafiti huu, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanya zoezi la kuorodhesha kaya katika maeneo yote 796 yaliyochaguliwa ili kupata orodha ya sasa ya kaya katika maeneo haya.

Hatua ya pili ya sampuli ilikuwa ni uchaguzi wa kaya 12 kutoka kwenye kila eneo lililochaguliwa. Wanakaya wote ambao kwa kawaida wanaishi katika kaya zilizochaguliwa na wageni waliolala katika kaya usiku wa kuamkia siku ya Utafiti bila kujali umri wao, walishiriki kutoa taarifa za Utafiti.

### 2.2 Maboresho

Katika kutekeleza HBS 2017-18, kulifanyika mabadiliko katika methodology ukilinganisha na tafiti zilizopita. Mabadiliko haya ni kama ifuatavyo:

#### *Mabadiliko ya kimuundo;*

- a) Sampuli iliboreshwa ili kutoa makadirio katika ngazi ya mikoa;
- b) Siku za ujazaji wa shajara zilipunguzwa kutoka siku 28 hadi 14;
- c) Kulikuwa na punguzo la idadi ya kaya zilizohojiwa kwa kila eneo kutoka kaya 24 hadi 12;
- d) Kulikuwa na mageresho ya kina na yaliyoboreshwa kwa bidhaa zinazonunuliwa au kutumiwa na kaya (COICOP);
- e) Matumizi ya vishikwambi (tablets) kwa ajili ya kukusanya taarifa wakati wa mahojiano;

*Ongezeko la moduli au maswali;*

- f) Moduli ya matumizi ya muda ili kupata viashiria vya jinsia vinavyohusiana na matumizi ya muda;
- g) Maswali yanayohusu huduma za mifuko ya jamii, bima na umiliki wa vitambulisho;
- h) Moduli ya hali ya usalama wa chakula kutoka FAO;
- i) Maswali ya umiliki wa mali na raslimali kwa jinsi;
- j) Maswali ya hali ya lishe kwa watoto chini ya miaka mitano; na
- k) Moduli ya vifo katika kaya.

## **2.3 Madodoso**

Utafiti wa HBS 2017-18 ulitumia madodoso ya aina sita yaliyoingizwa kwenye kishikwambi (Fomu I – V na VII) na shajara iliyokuwa kwenye karatasi (kijitabu cha kumbukumbu ya mapato na matumizi binafsi ya mwanakaya (Fomu namba VI)). Utafiti ulikusanya taarifa zifuatazo:

- a) **Fomu I:** Taarifa za kidemografia; hali ya uhai wa wazazi wa wanakaya; kujifungua na kunyonyesha; uraia na uhamaji/uhamiaji; elimu; kujua kusoma na kuandika; afya; ulemavu; bima; umiliki wa mali binafsi na nyaraka za utambulisho; viashiria vya hali ya ajira; hali ya biashara za wanakaya zisizo za kilimo; na mapato ya wanakaya yasiyo ya ujira;
- b) **Fomu II:** Taarifa za hali ya makazi ya kaya; huduma za maji na usafi; usafiri na mawasiliano; utalii; uwekezaji katika kaya; huduma za benki; matumizi ya kaya kwa kipindi kilichopita; na vifo katika kaya. Fomu hii ilikuwa pia na moduli ya TASAF na ya usalama wa chakula;
- c) **Fomu III:** Taarifa za kilimo ikiwa ni pamoja na mazao ya chakula, ufugaji wa wanyama, na usalama wa chakula;
- d) **Fomu IV:** Module ya Matumizi ya muda (kwa wanakaya wenye umri wa miaka 5 au zaidi);
- e) **Fomu V:** Shajara ya kaya kwa ajili ya kuorodhesha mapato na matumizi ya kila siku ya kaya kwa kipindi cha siku 14;
- f) **Fomu VI:** Shajara ya mwanakaya kwa ajili ya kuorodhesha mapato na matumizi ya kila siku ya mwanakaya kwa kipindi cha siku 14 kwa wanakaya wenye miaka mitano au zaidi; na
- g) **Fomu VII:** Upatikanaji wa huduma za kijamii (maeneo yaliyochaguliwa tu).



## **2.4 Utafiti wa Majaribio**

Mapitio ya madodoso na nyaraka nyingine za utafiti yalifanyika mwezi Desemba, 2017 mkoani Morogoro. Utafiti wa Majaribio ulifanyika mwezi Juni, 2018 katika mikoa ya Dodoma na Kilimanjaro.

## **2.5 Uorodheshaji wa Kaya, Ajira ya Wadadisi na Mafunzo**

Zoezi la uorodheshaji wa kaya katika maeneo 796 yaliyochaguliwa lilifanyika mwezi Julai, 2017 na kufuatiwa na uchaguzi wa kaya zilizohusika kwenye utafiti.

Jumla ya wadadisi 680 kutoka mikoa yote nchini waliajiriwa kwa ajili ya kuendesha mahojiano katika kaya zilizochaguliwa. Wadadisi hao walikuwa wanatoka katika maeneo yaliyochaguliwa kwa ajili ya utafiti.

Mafunzo ya wakufunzi yalifanyika wiki ya mwisho ya mwezi wa Oktoba, 2017 mkoani Dodoma. Mafunzo kwa wahusika wote wa zoezi la ukusanyaji wa taarifa za HBS (wadadisi, wasimamizi, wadhibiti ubora wa taarifa na wahariri) yalifanyika katika Jiji la Dodoma kwa siku 14 kuanzia tarehe 6 hadi 19 mwezi Novemba, 2017.

## **2.6 Ukusanyaji wa Taarifa**

Kazi ya ukusanyaji wa taarifa ilichukua miezi 12 mfufulizo kuanzia Desemba 2017 mpaka Novemba 2018. Kazi hii ilitumia vishikwambi vilivyounganishwa na mtandao kwa ajili ya kutuma taarifa Makao Makuu ya Ofisi - NBS kwa wakati.

## **2.7 Uchakataji wa Taarifa**

Uhariri na uchakataji wa taarifa za utafiti ulifanyika sambamba na ukusanyaji wa taarifa. Mfumo au Program ya *Survey Solutions* kutoka Benki ya Dunia ilitumika kuingiza taarifa kwenye vishikwambi, kufuatilia utendaji wa wadadisi na wasimamizi na kuhariri taarifa.

## **2.8 Mwitikio wa Utafiti**

Kati ya kaya 9,552 zilizochaguliwa, kaya 9,465 zilishiriki mahojiano na kufanya mwitikio wa Utafiti huu kuwa asilimia 99.

### 3 UPIMAJI WA KIWANGO CHA UMASKINI

Mbinu ya kuangalia **mahitaji ya msingi** hutumika kupima kiwango cha umaskini kwa Tanzania Bara. Njia hii inaonesha kipato cha chini kabisa anachohitaji mtu kwa ajili kukidhi mahitaji mbalimbali ya msingi. Hivyo, **mstari wa kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi ina maana ya kipato** kinachohitajika ili kukidhi mahitaji hayo.

Mstari wa kiwango cha umaskini wa chakula ni gharama ya matumizi yote ya kaya yanayohitajika kukidhi mahitaji ya chakula. Kiwango hiki pia hujulikana kama umaskini uliokithiri. Watu ambao wapo chini ya kiwango hiki wanatambulika kuwa na umaskini wa kupindukia.

#### 3.1 *Fahirisi za Umaskini*

Fahirisi za umaskini zinazotumika zaidi ni asilimia ya watu walio chini ya mstari wa kiwango cha umaskini, pengo la umaskini, na tofauti ya kipato miongoni mwa maskini. Kipimo cha umaskini ni takwimu ambayo inatafsiri mlinganisho wa kiashiria cha ustawi wa kaya na kiwango cha mstari wa umaskini kilichochaguliwa katika idadi kubwa ya watu au kikundi cha watu kwa ujumla. Kuna njia nyingi mbadala, lakini njia tatu zifuatazo ndizo zinazotumika zaidi:

##### **a) Kiwango cha Umaskini**

Kiwango cha Umaskini ni idadi ya watu maskini kati ya watu wote ambao kipato au matumizi yao yako chini ya mstari wa umaskini, yaani kipato chao hakikidhi mahitaji yao ya msingi. Kuna aina mbili za umaskini; **Umaskini wa Mahitaji ya Msingi** ambao ni kipimo cha umaskini kinachozingatia mahitaji ya chakula na mahitaji yasiyo ya chakula na **Umaskini wa Chakula** ambao ni jumla ya matumizi ya kila siku ya chakula.

##### **b) Pengo la Umaskini**

Fahirisi ya Pengo la Umaskini au Pengo la Umaskini inaonesha wastani wa umbali wa kaya kutoka kwenye mstari wa umaskini. Fahirisi ya Pengo la Umaskini inachukua wastani wa matumizi yanayopungua kutoka kwenye mstari wa umaskini kwa watu wote. Fahirisi ya Pengo la Umaskini inapatikana kwa kujumlisha upungufu wa umaskini wa watu (ukichukulia kwamba wale wasio maskini hawana upungufu wowote) na kugawanya kwa idadi ya watu wote. Kwa maana nyingine, inakadiria rasilimali zote zinazohitajika katika kuwaleta maskini wote kwenye mstari wa umaskini.

### c) Fahirisi ya Pengo la Umaskini Miongoni mwa Maskini

Fahirisi ya Pengo la Umaskini miongoni mwa maskini hupima tofauti miongoni mwa maskini. Uzito mkubwa huwekwa kwenye kaya ambazo ziko mbali na mstari wa umaskini. Tafiti zote zilizopita za hali ya umaskini Tanzania Bara na ripoti za umaskini katika nchi nyingi zinatumia fahirisi zote za umaskini hapo juu kuelezea umaskini.

## JINSI YA KUTENGENEZA MSTARI WA UMASKINI

Nchini Tanzania, umaskini unapimwa kwa kulinganisha matumizi ya kaya kwa mtu mzima katika mstari wa umaskini kwa kutumia takwimu za utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi. Matumizi ya kaya yanajumuisha vyakula, ikiwa ni pamoja na vyakula vilivyozalishwa na kaya na gharama za bidhaa mbalimbali na huduma (mfano mavazi, maji, umeme, usafirishaji, mawasiliano, afya na elimu). Matumizi haya hayajumuishi gharama za kodi ya nyumba na gharama nyinginezo zinazohusiana na nyumba (mfano ukarabati wa nyumba) na pia hayahusishi gharama za matukio ya kipekee (kama vile harusi, mazishi, n.k.) na gharama kubwa za manunuzi ya samani za kudumu (kama vile magari, luninga, n.k.).

**Mstari wa umaskini wa chakula** ni thamani ya fedha yenye kukidhi mahitaji ya kiwango cha chini cha aina mbalimbali za vyakula vyenye kufikia kiwango cha kilokalori 2,200 zinazohitajika kwa mlo wa mtu mzima kwa siku kwa mwezi kwa kuzingatia uwiano wa vyakula vilivyotumiwa na asilimia **10 hadi 50** ya watu wote. Gharama ya kukidhi matumizi ya chakula yenye kilokaloro 2,200 kwa mtu mzima mmoja kwa siku bila kujali eneo analotoka ni Shilingi za Kitanzania **1,109.53** au shilingi **33,748** kwa mwezi. Gharama hii inatokana na matumizi ya aina **251** za bidhaa za vyakula vinavyotumiwa zaidi Tanzania Bara. **Mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi** unahusisha wastani wa matumizi ya chakula pamoja na matumizi mengine yasiyo ya chakula kama vile nguo, usafiri, elimu, afya, n.k. ambacho kinafikia wastani wa Shilingi **49,320 kwa mtu mzima kwa mwezi**.

Njia kuu nne hutumika kupima hali ya umaskini: njia ya kwanza ni kwa kutumia **Umaskini wa Mahitaji ya Msingi** ambayo hupima uwiano wa watu ambao matumizi yao kwa mwezi kwa mtu mzima yako chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi. Njia ya pili hutumia **Umaskini wa Mahitaji ya Chakula (umaskini uliokithiri)** ambayo unapima uwiano wa watu wanaoishi chini ya **Mstari wa Umaskini wa Mahitaji ya Chakula**. Njia ya tatu hutumia **Pengo la umaskini** (poverty gap) ambalo huonesha wastani wa umbali wa kaya zenye umaskini uliokithiri kutoka kwenye mstari wa umaskini. Fahirisi ya pengo la umaskini inachukua wastani wa matumizi yanayopungua kutoka kwenye mstari wa umaskini kwa watu wote maskini. Fahirisi ya pengo la umaskini inahusisha wastani wa upungufu wa matumizi ya watu maskini kutoka kwenye mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi na kugawanywa kwa idadi ya watu katika nchi. Fahirisi ya pengo la umaskini husaidia kuonesha kiasi cha rasilimali kinachohitajika kuondoa watu katika umaskini kwa kuzingatia kuwa watu wote maskini wana upungufu wa mahitaji uliosawa kutoka kwenye mstari wa umaskini. **Umaskini wa kupindukia (severity of poverty)** hunapima kwa pamoja wastani wa umbali wa kaya maskini kutoka kwenye mstari wa umaskini mahitaji ya msingi na tofauti ya matumizi miongoni mwa watu maskini.

## 4 VIASHIRIA MUHIMU

### 4.1 Muundo wa Matumizi

Utafiti wa HBS 2017-18 unaonesha kuwa wastani wa matumizi ya kaya moja kwa mwezi kwa Tanzania Bara ni shilingi 416,927. Kiwango hiki cha matumizi ni kikubwa kwa Maeneo ya Mijini (TZS 534,619) kuliko Maeneo ya Vijijini (TZS 361,956).

Kuna tofauti kubwa ya wastani wa matumizi ya kaya kwa mwezi katika mikoa ya Tanzania Bara. Mkoa wa Dar es Salaam una wastani wa juu kabisa wa matumizi (TZS 720,946) na Mkoa wa Rukwa (TZS 268,041) una wastani wa chini kabisa wa matumizi (Jedwali Na. 4.1) ya kaya kwa mwezi. Mwenendo huu unaonekana pia katika wastani wa matumizi ya mtu mmoja mmoja ya chakula, bidhaa zisizo za chakula na jumla ya matumizi yote ya mtu mzima mmoja kwa mwezi.

**Jedwali Na. 4.1:** Wastani wa Matumizi ya Kaya na Wastani wa Matumizi ya Mtu Mzima kwa Mwezi kwa Eneo, Mkoa na Aina ya Wastani ya Matumizi, Tanzania Bara, HBS 2017-18

Kipengele	Wastani wa matumizi ya kaya kwa Mwezi (shilingi)	Aina ya Wastani ya Matumizi (shilingi) ya Mtu Mzima kwa Mwezi		
		Chakula	Zisizo za Chakula	Jumla
<b>Eneo</b>				
Vijijini	361,956	44,473	31,593	76,065
Mijini	534,619	58,835	76,694	135,529
<b>Mkoa</b>				
Dodoma	356,357	51,007	39,694	90,700
Arusha	457,258	50,261	58,908	109,169
Kilimanjaro	496,661	67,457	57,014	124,470
Tanga	385,116	51,709	42,851	94,559
Morogoro	405,535	49,751	52,202	101,953
Pwani	402,107	58,532	52,495	111,027
Dar es Salaam	720,946	70,966	115,639	186,605
Lindi	270,850	46,844	28,000	74,844
Mtwara	346,447	52,387	45,702	98,090
Ruvuma	350,782	47,626	44,367	91,993
Iringa	307,315	45,731	38,078	83,810
Mbeya	350,620	56,247	44,022	100,269
Singida	354,533	42,990	26,383	69,373
Tabora	423,218	41,473	37,618	79,091
Rukwa	268,041	35,169	24,547	59,716
Kigoma	273,625	34,353	29,446	63,799
Shinyanga	456,246	45,825	24,199	70,024
Kagera	294,275	39,334	28,246	67,580
Mwanza	390,236	42,439	31,563	74,003
Mara	463,417	49,356	37,038	86,394
Manyara	395,340	44,593	38,486	83,079
Njombe	400,727	51,674	52,983	104,657
Katavi	489,780	45,819	25,138	70,957
Simiyu	452,304	41,416	29,835	71,251
Geita	417,713	37,865	29,696	67,561
Songwe	455,973	46,814	40,836	87,650
<b>Jumla (Wastani)</b>	<b>416,927</b>	<b>49,045</b>	<b>45,952</b>	<b>94,997</b>

## 4.2 Mstari wa Umaskini

Mstari wa umaskini wa chakula kwa Tanzania bara kwa kutumia matokeo ya HBS 2017-18 ni shilingi 33,748 kwa mtu mzima mmoja kwa mwezi na mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi ni shilingi 49,320 (Jedwali 4.2).

**Jedwali Na. 4.2:** Mstari wa Umaskini wa Chakula na Mahitaji ya Msingi (shilingi) kwa Mtu Mzima kwa mwezi, Tanzania Bara, HBS 1991-92 hadi 2017-18

Mwaka	Mstari wa Umaskini wa Mahitaji ya Msingi (TZS kwa mwezi)	Mstari wa Umaskini wa Chakula (TZS kwa mwezi)
1991-02	2,777	2,083
2000-01	7,253	5,295
2007	13,998	10,219
2011-12	36,482	26,085
2017-18	49,320	33,748

**Mwenendo:** Mstari wa umaskini wa chakula umeongezeka kutoka shilingi 26,085 mwaka 2011-12 hadi 33,748 mwaka 2017-18, na mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi umeongezeka kutoka shilingi 36,482 mwaka 2011-12 hadi 49,320 mwaka 2017-18.

## 4.3 Kiwango na Kina cha Umaskini

Utafiti wa HBS 2017-18 umeonesha kuwa asilimia 26.4 ya watu wa Tanzania Bara wana umaskini wa mahitaji ya msingi (Jedwali Na. 4.3). Umaskini wa mahitaji ya msingi ni mkubwa vijijini (31.3%) kuliko mijini (15.8%). Mkoa wa Rukwa una kiwango kikubwa zaidi cha umaskini wa mahitaji ya msingi (45.0%) na Mkoa wa Dar es Salaam (8.0%) una kiwango kidogo zaidi.

Vile vile, asilimia 8.0 ya watu Tanzania Bara wanaishi katika umaskini wa chakula. Umaskini huu ni mkubwa vijijini (9.7%) kuliko mijini (4.4%). Katika ngazi ya mkoa, umaskini wa chakula ni mkubwa zaidi katika mkoa wa Rukwa (19.8%) na ni ndogo zaidi katika Mkoa wa Kilimanjaro (2.1%).

Wastani wa kina cha umaskini wa mahitaji ya msingi katika ngazi ya taifa ni asilimia 6.2 na wa kina cha umaskini wa mahitaji ya chakula ni asilimia 1.4.

Kipimo cha **Fahirisi ya Pengo la Umaskini** kinaweza kusaidia maafisa mipango na wasimamiaji wa sera mbalimbali za kijamii kujua ni kiasi gani cha fedha kitaweza kuwatoa watu maskini katika hali hiyo ili wafikie mstari unaopima kiwango cha umaskini. Kiasi kinachohitajika hupatikana kwa kuzidisha pengo la umaskini nchini (0.062) na idadi ya watu waishio katika kaya binafsi (milioni 52, 691,314) pamoja na kiwango cha mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi (shilingi 49,320). Kwa

